

Telegram: "MIFUGO"

Simu: +255 26 2322610

Nukushi: +255 262322613
2861908

E-Mail: ps@mifugo.go.tz

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA MIFUGO NA UVUVI**



Mji wa Serikali Mtumba,

Mtaa wa Ulinzi,

S.L.P. 2870,

Dodoma, Julai 08, 2026

TAARIFA KWA UMMA

**UTOAJI WA VIBALI VYA VITOTOLESHI VYA VIFARANGA
VYA SAMAKI (FISH HATCHERY)**

Serikali kupitia Wizara ya Mifugo na Uvuvi inataarifu wananchi wote wenye vitotoleshi vya vifaranga vya samaki (*Fish Hatchery*) wanatakiwa kuwa na kibali stahiki kinachokubalika kisheria kwa ajili ya uendeshaji wa shughuli hiyo.

Wizara inaendelea na jukumu la kusimamia shughuli za ukuzaji viumbemaji (*aquaculture*) nchini kwa mujibu wa Sheria ya Uvuvi, Sura 279 na Kanuni za Ukuzaji Viumbemaji za Mwaka 2024.

Kwa kuzingatia jukumu hilo, Kibali hicho kinapatikana kupitia mfumo wa FIRGIS <https://fircis.mlf.go.tz/> hivyo wamiliki wa vitotoleshi vya vifaranga vya Samaki kote nchini wanapaswa kukamilisha taratibu za kupata kibali husika **kabla au ifikapo tarehe 31 Agosti 2026**. Wizara inasisitiza kuwa baada ya muda huo kuisha, hatua za kisheria zitachukuliwa dhidi ya mtu yeyote atakayebainika kuendesha kitotoleshi bila kuwa na kibali.

Kwa maelezo zaidi wasiliana na Bw. Ayubu Mwasote kwa simu **+255 766 029 961** na barua pepe ayubu.mwasote@mlf.go.tz

**Imetolewa na:
Idara ya Ukuzaji Viumbemaji
Wizara ya Mifugo na Uvuvi
S.L.P 2847
Dodoma**